

# Mwongozo wa Barakoa Wakati wa COVID-19

## Muhtasari wa Mabadiliko ya tarehe 12 Septemba, 2022

- Taarifa iliyoongezwa kwenye viwango tofauti vyta ulinzi unaotolewa na barakoa na vipumuzi
- Imesasishwa ili kuendana na [mapendekezo ya barakoa ya Centers for Disease Control and Prevention \(CDC, Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa\)](#) kwa ajili ya usafiri wa umma wa ndani ya chombo.
- Mapendekezo yaliyosasishwa ya wakati ambapo barakoa zinfaa kuvaliwa katika [mazingira yasiyo ya huduma ya afya ambayo yana umati wa watu](#)
- Mapendekezo yaliyosasishwa ya wakati ambapo [umma wa kawaida](#) wanafaa kuva barakoa ndani ya nyumba, kwa mujibu wa Viwango vya CDC vya COVID-19 katika Jamii

## Utangulizi

Ukivaa barakoa au kipumuzi (yaani barakoa maalum za kuchuja kama vile N95), unasaidia kuwalinda wengine walio karibu na wewe sawa na wewe pia. Kuva barakoa au kipumuzi kunaweza kupunguza msambao wa COVID-19, na kuokoa maisha na kuendelea kufungua uchumi. Mikakati iliyojumuishwa, kama vile [kupokea chanjo zote](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) na kuva barakoa na vipumuzi, kunaweza kusaidia kuzuia maradhi makali na kupunguza mzigo kwenye mfumo wa huduma ya afya.

Unafaa kuva [barakoa au kipumuzi](#) kinachokutoshea vizuri na chenyе ubora wa juu zaidi (lugha nyingine za ziada zinapatikana) ambacho unaweza kupata. Vikivaliwa vizuri, vipumuzi [vilivvoidhinishwa na National Institute for Occupational Safety and Health \(NIOSH, Taasisi ya Kitaifa ya Usalama wa Kikazi na Afya\)](#) (Kiingereza pekee) (kama vile barakoa za N95) hutoa ulinzi mkali zaidi, vikifuatwa na vipumuzi vya kimataifa (kama vile KN95 na KF94) na barakoa za upasuaji, na kisha barakoa za uso zilizotengenezwa kwa nguo. Iwapo [upo katika hatari ya ugonjwa mkali wa COVID-19](#), tafuta ushauri kutoka kwa mhudumu wako wa afya kuhusu iwapo unafaa kupimwa kuona kama unaweza kutumia kipumuzi kilichoidhinishwa na NIOSH au iwapo unafaa kuzingatia chaguo nyingine za vipumuzi ambazo hazihitaji kupimwa kama unaweza kuvitumia. Kwa maelezo zaidi kuhusu kupima kama unaweza kutumia kipumuzi na kuchagua barakoa, tembelea [ukurasa wa wavuti wa Washington State Department of Labor and Industries \(L&I, Idara ya Leba na Viwanda katika Jimbo la Washington\) kuhusu kuva barakoa kwa kupenda kwako](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana).

Kwa maelezo zaidi kuhusu aina tofauti za barakoa na vipumuzi na jinsi ya kuboresha kutoshea, tazama [aina za barakoa na vipumuzi](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) [Ukurasa huu wa wavuti](#) (Kiingereza pekee) unatoa taarifa nyingine kuhusu jinsi ambavyo aina tofauti za barakoa na vipumuzi huchuja chembechembe, ikiwa pamoja na wakati ambapo marekebisho yanafanywa kwa barakoa ili kuboresha kutoshea. Watu ambaeo hawawezi kuva barakoa kwa sababu ya sababu za kukua, kitabia, au kimatibabu wanaweza kutumia ngao ya uso iliyo na kamba. Hizi pia inaweza kutumika na watoto walio katika vituo vya utunzaji, kambi ya mchana, na mazingira ya

K-12 iwapo barakoa inayotoshea vizuri imetumika. **Inafaa kufahamiwa, hata hivyo, hizi hazitoi kiwango sawa cha ulinzi kwa anayevalia kama barakoa au kipumuzi kinachotoshea vizuri.** Tazama mwongozo wa barakoa wa Washington State Department of Health (WA DOH, Idara ya Afya katika Jimbo la Washington,) [K-12 Schools, Child Care, Early Learning, Youth Development, and Day Camp Programs \(Shule za K-12, Utunzaji wa Mtoto, Masomo ya Chekechea, Maendeleo ya Mtoto, na Programu za Kambi ya Mchana\)](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana). Pia tazama [Uzingatiifu wa CDC wa vikundi maalum nya watu](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana). DOH inapendekeza kutotumia barakoa zilizo na valvu au venti za kutumiwa kupumua anje, barakoa zenye nguo ya safi moja, bbandana yenye safu moja, au geita.

Vipumuaji vyenye valvu za kupumua nje vinaweza kutumika kwa mujibu wa mwongozo uliochapishwa na [L&I](#) (Kiswahili only).

Tafadhalni tembelea [ukurasa wa wavuti kuhusu barakoa wa DOH](#) (Kiingereza pekee) ili kupata orodha ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara.

Katika sehemu zote za waraka huu zilizosalia, barakoa inatumika kurejelea barakoa na vipumuaji.

## Majukumu ya Sasa na Amri za Afya

Amri za sasa za umma zinahitaji barakoa katika [mazingira ya huduma ya afya](#), magereza ya watu wazima, na korokoro za watu wazima. Mamlaka ya afya ya umma huenda yakahitaji barakoa katika baadhi ya hali, kama vile mkurupuko.

### Amri ya Department of Health katika Jimbo la Washington

[Amri ya Barakoa ya Katibu wa Afya](#) (Kiingereza pekee) inahitaji kuvala barakoa katika baadhi ya mazingira, bila kujali hali ya chanjo:

- [Mazingira ya Huduma ya Afya](#)
- Vituo nya gereza na korokoro ya watu wazima wakati ambapo kaunti yenye kituo hicho kipo ina [Kiwango cha CDC cha Kati au Juu cha COVID-19 katika Jumuiya](#) (Kihispania kinapatikana)

Kuna hali kidogo zinazoruhusiwa kutofuata hitaji hili; hizi zinaweza kupatikana katika [Amri](#) (Kiingereza pekee). Waajiriwa na wageni wote, pamoja na wataalamu wa huduma ya afya, wanahitajika kuvala barakoa wakiwa ndani ya nyumba katika [mazingira a huduma ya afya](#). Kila mtu anawajibikia kufuata amri hizo; biashara pia zina majukumu ya kutekeleza amri hii na waajiriwa na wateja wao.

### Imebatilishwa: Amri ya Shirikisho

Kuanzia tarehe 18 Aprili 2022, kutokana na amri ya korti, Amri ya CDC inayohitaji barakoa katika usafiri wa umma na vituo nya uchukuzi haifanyi kazi tena. Hata hivyo, barakoa zinasalia kuwa zana muhimu ili kuhakikisha usafiri na uchukuzi wa umma ni salama kwa kila mtu. [Kwa kufuata amri za CDC](#) (lugha nyingine zinapatikana), WA DOH inapendekeza wafanyakazi na wasafiri walio na umri wa miaka miwili au zaidi wavae barakoa katika mazingira yote ya usafiri wa ndani ya nyumba, ikiwemo vituo nya uchukuzi. Tazama [Mazingira ya Usafiri wa Umma](#) kwa maeleo zaidi.

### Tangazo la Gavana wa Jimbo la Washington

Taarifa kuhusu majukumu ya biashara kwa wateja na waajiriwa imeorodheshwa katika [Proclamation 20-25.19 COVID-19 Washington Ready \(Tangazo la Gavana la 20-25.19 Kuhusu Utayari wa COVID-19 katika Washington\)](#) (Kiingereza pekee) na [Proclamation 21-08 – Safe Workers \(Tangazo la 21-08 - Wafanyakazi Salama\)](#) (Kiingereza pekee).

### **Washington State Labor and Industries (L&I) na Tangazo la Gavana**

Ijapokuwa barakoa kawaida hazihitajiki katika maeneo kadhaa ya kufanya kazi kulingana na Tangazo la Gavana lililoordheshwa hapo juu, waajiri wanaendelea kuwa na jukumu la kufuata [Mahitaji na Mwongozo wa Kuzuia COVID-19](#) ya L&I (Kiingereza pekee). Isitoshe, biashara za kibinaksi zinaweza kuchagua kuhitaji barakoa na wageni wanafaa kuheshimu [kanuni za chumba](#). Kupitia [Proclamation 21-08 – Safe Workers ya Gavana \(Tangazo la Gavana la 21-08 - Wafanyakazi Salama\)](#) (Kiingereza pekee), wafanyakazi wana haki ya kuvala barakoa katika maeneo ya kazi. [Washington Administrative Code \(WAC, Msimbo wa Utawala katika Washington\) 296-62-609](#) (Kiingereza pekee) hulinda haki ya mfanyakazi ya kuvala barakoa wakati wa dharura ya afya ya umma. Kwa mujibu wa [WAC 296-62-609](#) (Kiingereza pekee), waajiri hawawezi kuwazuia waajiriwa kuvala barakoa, vipumuzi, au vifaa vingine vya kibinaksi vya kujilinda isipokuwa ikitiruhusiwa na sheria. Tazama [Uzuiaji wa COVID-19 wa L&I: Kuchagua Kuvala Barakoa Kazini Wakati Ambapo Huhitajiki Kuvala](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) kwa maelezo zaidi.

### **Taasisi na Maafisa wa Afya ya Umma ya Ndani**

Maafisa wa afya ya ndani wana mamlaka ya kutoa amri za afya ili kudhibiti magonjwa ndani ya mipaka yao. Amri hizi huenda ni za shuruti zaidi ya amri za jimbo zima lakini huenda hazishurutishi zaidi. Angalia kwa [mamlaka yako ya ndani ya afya](#) (Kiingereza pekee) na ufuate amri zote za afya zinazotumika katika eneo hilo.

### **Mapendekezo**

Fafuatayo ni mapendekezo ya jumla ya afya ya umma pamoja na mahitaji maalum yaliyo hapo juu.

### **Mazingira ya Usafiri wa Umma**

WA DOH inapendekeza kuwa wafanyakazi na abiria walio na umri wa miaka miwili au zaidi wavae barakoa au kipumuzi kinachowatoshea vizuri sana katika [mazingira ya usafiri ya ndani ya chombo](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana), ikiwemo vyombo vya usafiri (kama vile ndege, mabasi, treni, feri, teksi, kutumia gari pamoja, na usafiri wa kimatibabu usio wa dharura) na vituo (kama vile uwanja wa ndege, vituo vya basi au feri, vituo vya treni, na vituo vya baharini). Haya ni mazingira ambayo watu wengi hupitia, na yanaweza kuwa na watu wengi na/au kuwa na mzunguko duni wa hewa (kama vile njia za kuabiri ndege katika kituo cha ndege). Wasafiri na wafanyakazi wanaweza kujilinda na kuwalinda walio karibu nao kwa kuvala barakoa au kipumuzi kinachowatoshea vizuri ili kusaidia kuweka salama kwa kila mtu safari na usafiri wa umma. Tafadhali ona [mwongozo wa CDC kuhusu kutumia barakoa za uso katika mazingira ya usafiri wa umma](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) kwa maelezo, lakini ukumbuke kuwa mahitaji ya awali sasa ni mapendekezo. Tazama [Mahitaji na Mwongozo wa Kupunguza Msambao wa COVID-19 katika K-12 Schools, Child Care, Early Learning, Youth Development, and Day Camp Programs \(Shule za K-12, Utunzaji wa Mtoto, Chekechea, Ukuaji wa Vijana, na Programu za Kambi ya Mchana\) \(wa.gov\)](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) ili kupata

mwongozo wa barakoa kwenye mabasi ya shule. WA DOH huwahimiza waendeshaji wa usafiri wa umma kusaidia watu wote kucaa barakoa.

### Kucaa Barakoa katika Mazingira ya Huduma ya Afya

Barakoa lazima zivaliwe katika mazingira ya huduma ya afya kwa mujibu wa [Katibu wa Amri ya Barakoa ya Afya](#) (Kiingereza pekee). Mazingira yote ya huduma ya afya yanaweza kufikia vifaa vya kujilinda kibinafsi na kutafuta mwongozo wa udhibiti katika [Mapendekezo ya Kaimu ya Uzuiaji na Udhibiti wa Maambukizo ya SARS-CoV- 2 katika Mazingira ya Huduma ya Afya, DOH 420-391 \(wa.gov\)](#) (Kiingereza pekee).

### Mapendekezo ya Kucaa Barakoa ya Mazingira ya Umati Yasiyo ya Huduma ya Afya

Utumiaji wa barakoa ndani ya nyumba inapendekezwa kwa watu walio na umri wa miaka miwili au zaidi wakati ambapo [Kiwango cha CDC cha COVID-19 katika Jamii](#) (Kihispania kinapatikana) kipo wastani au juu katika mazingira yanayofuata:

- [Wavuti wa mtoaji huduma asiyе na makao](#) (Kiingereza pekee)
- [Mazingira ya kibiashara ya baharini](#) (Kiingereza pekee) (k.v., vyombo vya samaki wa kibiashara, meli za mizigo, meli za kimataifa).
- Mazingira ya kazi yenye umati mkubwa ambapo kukaa mbali na wengine hakuwezekani kwa sababu ya hali ya kazi, kama vile katika maghala, viwanda, na vituo vya uwekaji chakula kwenye mikebe na usindikaji wa nyama, na usafiri unaotolewa na mwajiri
- Maeneo ya makao yanayoshirikiwa yenye vifaa vya kuishi vya umati mkubwa (si vyumba vya kulala), pamoja na vituo vya kutoka kazini, nyumba ya mpito, marekebisho ya watoto au vituo vya wafungwa, na nyumba ya muda ya mfanyakazi
- Ndani ya nyumba katika mazingira ambapo watu wamefungwa katika magereza ya watu wazima, jela za watu wazima, vituo vya marekebisho ya watoto, au vituo vya kifungo cha watoto wapo (mfano, vyumba vya mahakama).
  - Kumbuka kuwa Katibu wa Amri ya Afya [anahitaji](#) watu walio na umri wa miaka mitano na zaidi wavae barakoa katika magereza ya watu wazima na vituo vya kifungo wakati ambapo [Kiwango cha CDC cha COVID-19 katika Jamii](#) (Kihispania kinapatikana) kipo wastani au juu.
  - Vituo vya marekebisho vinapendekezwa pia vizingatie kucaa barakoa wakati ambapo [vipengele vya kiwango cha kituo](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) vinajumuisha ongezeko la hatari.

Watu wanaoishi au kufanya kazi katika mazingira yaliyo hapo juu wanafaa kufuata mapendekezo sawa na umma kwa jumla wakati ambapo hawako katika mazingira haya (mfano, wakiwa nje katika jamii).

Mazingira yasiyo ya huduma ya afya (kama vile biashara na mashirika) yanaweza kuhitaji kucaa barakoa katika vituo vyao. Mazingira haya yanafaa kuzingatia kila moja kati ya vipengele vifuatavyo wanapoamua kama watahitaji barakoa katika mazingira yao:

- Uwezo wa kudhurika kwa watu katika mazingira hayo
  - Watu ambao [hawajapokea chanjo zote](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) za COVID-19 wanaweza kuambukizwa COVID-19 zaidi na hata kuwa na maradhi kali.

- Watu walio na [hali fulani za kiafya](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) wapo katika hatari ya juu ya maradhi makali ya COVID-19.
- Ubora wa mzunguko wa hewa katika mazingira hayo - tazama [Mzunguko wa Hewa na Ubora wa Hewa wa Kupunguza Msambao wa Magonjwa Yanayosambazwa kwa Hewa](#) (Kiingereza pekee) na [Kampeni ya Hewa Safi katika Majengo, Environmental Protection Agency \(EPA, Shirika la Ulinzi wa Mazingira\)](#) (Kiingereza pekee) ili kupata maelezo na chaguo za mzunguko wa hewa, ikijumuisha kwa vituo vilivyo na visivyo na mifumo ya HVAC ya kuweka joto, mzunguko wa hewa, na udhibiti wa hewa
- Uwezo wa watu kukaa mbali na wengine katika mazingira hayo
- Mkurupuko unaoshukiwa au uliothibitishwa wa COVID-19 katika mazingira hayo
  - Utumiaji wa barakoa ndani ya nyumba unapendekezwa zaidi kukiwa na mkurupuko katika mazingira yasiyo ya huduma ya afya.

[Kiwango cha CDC cha COVID-19 katika Jamii](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) kikiwa juu, CDC na DOH zinapendekeza kuwa watu wote wavae barakoa ndani ya nyumba, licha ya hali ya chanjo. Uwekaji haufai kufanya watu wasivae barakoa wakichagua kufanya hivyo. Tazama ifuatayo ili kupata mapendekezo ya kuva barakoa kibinafsi na mambo ya kuzingatia yanayoegemea hatari.

#### [Mapendekezo ya Kibinafsi ya Barakoa](#)

Watu walio na dalili, waliopatikana na maambukizo, au walio na mfiduo wa mtu aliyeambukizwa COVID-19 wanafaa kuva barakoa yenyе ubora wa juu, kwa mujibu wa [Jambo la kufanya iwapo utapatikana na maambukizo ya COVID-19](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana), [Majedwali ya Uamuzi wa Dalili ya COVID-19](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana), na [Jambo la kufanya ikiwa huenda ulikuwa na mfiduo na mtu aliye na COVID-19](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana). Watu lazima wavae barakoa iwapo inahitajika katika mazingira waliyomo kulingana na [Ruhusa za Sasa na Amri za Afya](#).

Katika hali yoyote, unaweza kuchagua kuva barakoa. Zingatia vipengele vifuatavyo unapoamua kama utavaa barakoa:

- Hali yako ya chanjo na hali ya chanjo ya walio karibu nawe. Watu ambao [hawajapokea chanjo zote](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) za COVID-19 na busta wanaweza kuambukizwa COVID-19 zaidi na hata kuwa na maradhi kali.
- [Hali zako za afya](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) na hali za afya za walio karibu nawe walio katika hatari ya juu ya ugonjwa mkali wa COVID-19. Watu walio na hali fulani za kiafya wanaweza kuambukizwa COVID-19 zaidi na hata kuwa na maradhi kali.
- Sifa za mazinira uliyomo (k.m, umati mkubwa, mzunguko duni wa hewa, ndani ya nyumba).
- [Kiwango cha CDC cha COVID-19 katika Jamii](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana)
  - Viwango vya ugonjwa katika jamii vikiwa juu, CDC na WA DOH zinapendekeza kuva barakoa ndani ya nyumba, licha ya hali ya chanjo.
  - Viwango vya jamii vya ugonjwa vikiwa [wastani au juu](#), CDC na WA DOH zinapendekeza kuwa watu walio katika [hatari ya juu ya kuwa wagonjwa mno](#) (lugha nyingine za ziada zinapatikana) kwa sababu ya COVID-19 wavae barakoa

au kipumuzi chenye ubora wa juu wakiwa ndani ya nyumba au katika umma. Watu walio na mtagusano katika kaya au kijamii na mtu aliye katika hatari ya juu zaidi ya kuwa mgonjwa mno wanafaa kuzingatia kuvalaa barakoa yenye ubora wa hali ya juu wakiwa ndani ya nyumba na wao.

## Taarifa na Rasilimali Zaidi za COVID-19

Pata habari kila mara kuhusu [hali ya sasa ya COVID-19 katika Washington](#) (Kiingereza pekee), [matangazo ya Gavana Inslee](#) (Kiingereza pekee), [dalili](#) (lughu nyingine za ziada zinapatikana), [inavyosambaa](#) (lughu nyingine za ziada zinapatikana), [jinsi na wakati ambao watu wanafaa kupimwa](#) (Kihispania kinapatikana), na [mahali pa kupata chanjo](#) (Kihispania kinapatikana). Tazama [Maswali Yanayoulizwa Mara Kwa Mara](#) (Kiingereza pekee) ili kupata maelezo zaidi.

Asili/kabila au uraia kivyake haiwaweki katika hatari ya juu ya COVID-19. Hata hivyo, data inaonyesha kuwa jamii za watu wasio wazungu haziathiriwi zaidi na ugonjwa wa COVID-19. Hii ni kwa sababu ya athari za ubaguzi wa rangi, na hasa, ubaguzi wa rangi wa kimfumo, ambao huacha baadhi ya makundi ya watu na fursa chache za kujilinda na kulinda jamii zao.

[Unyanyapaa hautasaidia kupigana na ugonjwa](#) (Kiingereza pekee). Shiriki taarifa sahihi na wengine ili kuzuia uvumi na taarifa ya uongo dhidi ya kusambaa.

- [WA State Department of Health Mkurupuko wa Virusi Vipya vya Korona vya 2019 \(COVID-19\)](#) (Kiingereza pekee)
- [Mwitikio wa Virusi vya Korona katika WA State \(COVID-19\)](#) (lughu nyingine za ziada zinapatikana)
- [Tafuta Idara au Wilaya yako ya Ndani ya Afya](#) (Kiingereza pekee)
- [CDC Virusi vya Korona \(COVID-19\)](#) (lughu nyingine za ziada zinapatikana)

**Una maswali zaidi?** Piga simu kwa nambari yetu ya Taarifa ya COVID-19 kupitia **1-800-525-0127**. Saa za kupiga simu:

- Jumatatu saa 12 asubuhi hadi saa 4 usiku.
- Jumanne hadi Jumapili kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni.
- [sikukuu za jimbo zinazofuatiiliwa](#) (Kiingereza pekee) kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni.

Kwa huduma za ukalimani, **bofya #** wakipokea simu na **useme lughu yako**. Kwa maswali kuhusu afya yako mwenyewe, au matokeo ya kipimo, tafadhali wasiliana na mhudumu wa afya.

Ili kuomba hati hii katika muundo mwingine, piga simu kwa 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 ([Washington Relay](#)) au tuma barua pepe [civil.rights@doh.wa.gov](mailto:civil.rights@doh.wa.gov).

## Kiambatisho A:

### Mazingira ya Idara ya Afya

Kulingana na [Secretary of Health's Mask Order \(Amri ya Barakoa ya Katibu wa Afya\)](#) (Kiingereza pekee), Mazingira ya huduma ya afya na mazingira ya utoaji wa huduma ya utunzaji kwa muda mrefu ni mazingira yoyote ya umma au kibinafsi ambayo yanatumika kimsingi katika uwasilishaji wa huduma za afya kwa mtu binafsi kwa watu, na baadhi ya mambo yasiyojumuishwa. Iwapo lipo katika kituo kinachotumika kimsingi kuwasilisha huduma za

utunzaji wa afya, kama vile hospitali, basi kituo kizima cha afya ni mazingira ya utunzaji wa afya au mazingira ya utunzaji wa muda mrefu, na barakoa ni lazima zivaliwe wakati wote ukiwa kwenye kituo, chini ya bila kujumuisha mambo katika amri ya kutovaa barakoa. Iwapo upo katika kituo ambacho kimsingi kinatumika kwa madhumuni mengine, kama vile famasia ndani ya duka la mboga au ofisi ya muuguzi wa shule, mazingira ya huduma ya afya au mazingira ya muda mrefu ya utunzaji wa afyayanajumuisha maeneo pekee yanayotumika kimsingi katika kuwasilisha huduma ya afya, lakini si maeneo mengine ya kituo hicho. Barakoa lazima zivaliwe katika maeneo yanayotumika kimsingi kwa ajili ya utoaji wa utunzaji wa afya, chini ya bila kujumuisha mambo katika amri ya kutovaa barakoa. Isipokuwa ikiwa hajatajwa hapa chini, wahudumu wa afya wanajumuisha watu walio na sifa zilizoorodheshwa katika orodha ya [Mahitaji ya Utoaji Sifa ya Mtaalamu wa Huduma ya Afya](#) (Kiingereza pekee) sawa na watu walioruhusiwa na sheria kutoa huduma za afya bila kuwa na sifa. **Waajiriwa na wageni wote, pamoja na wataalamu wa huduma ya afya, wanahitajika kuвая barakoa wakiwa ndani ya nyumba katika mazingira a huduma ya afya.**

Ifuatayo ni orodha isiyo jumuishi ya mazingira ya huduma ya afya na mazingira ya utunzaji wa muda mrefu:

- Vituo vya utunzaji wa kina, vikiwa pamoja na, japo havina kikomo kwa, hospitali;
- Vituo vya utunzaji wa kina kwa muda mrefu;
- Vituo vya marekebisho ya wagonjwa waliolazwa;
- Vituo vya afya ya kitabia kwa waliolazwa, vikiwemo, japo havina kikomo kwa, vituo vya tathmini na matibabu, vituo vya matibabu ya wakazi, vituo salama vya kutoa sumu;
- Vituo vya huduma ya utunzaji vya muda mrefu, vikiwemo, japo havina kikomo kwa, makao ya wagonjwa, vituo vya wanaosaidiwa kuishi, makao ya familia ya watu wazima, mazingira ambapo huduma na misaada ya makao ya jamii iliyoidhinishwa inatolewa, na vituo vya huduma vilivoyezeshwa;
- Kliniki zisizo za mahali mmoja au magari mengine ambapo huduma ya afya hutolewa;
- Vituo vya wanaotibiwa na kurudi nyumbani, japo havina kikomo kwa, vituo vya matibabu ya saratani, ofisi za madaktari, na vituo vya afya ya kitabia (pamoja na ofisi za wanasaikolojia, washauri wa afya ya kiakili, na wataalamu wa utumiaji wa dawa ya kulevya);
- Vituo vya matibabu ya meno;
- Vituo vya kupima macho na uwezo wa kuona mbali;
- Famasia (bila kujumuisha maduka ya rejareja);
- Ofisi za kukanda mwili (hii inajumuisha maeneo ambapo ukandaji wa mwili hutolewa ndani ya mazingira yasiyo ya huduma ya afya kama vile spa na vituo vya ustawi);
- Ofisi za utabibu wa maungo;
- Matendo ya ukunga na vituo vya kuzaa;
- Vituo vya kujitenga na/au karantini;
- Vituo vya upasuaji wa kusogezeka;
- Vituo vya utunzaji wa dharura;
- Vituo vya utunzaji wa hospitali ya wagonjwa mahututi; na
- Mazingira ambapo utunzaji wa afya nyumbani, utunzaji nyumbani, utunzaji wa kibinafsi, au huduma za utunzaji wa wagonjwa mahututi hutolewa na wahudumu wanaolipwa.

Mazingira ya huduma ya afya na mazingira ya utunzaji wa muda mrefu haujumuishi:

- Mazingira ambapo matukio ya spoti na mashabiki au umati mwingine upo (pamoja na wakati ambapo wakufunzi waliofuzu wa riadha wanatoa utunzaji kwa wachezaji), kando na maeneo ambayo kimsingi yanatumika kutoa huduma za utunzaji wa afya, kama vile maeneo yaliyotengwa ya huduma ya kwanza (ambayo ni mazingira ya huduma ya afya);
- Makao yenyе leseni ya Department of Children, Youth & Families (DCYF, Idara ya Watoto, Vijana na Familia) ambayo kimsingi hayatoi huduma za utunzaji wa afya;
- Vituo vya utafiti ambapo huduma ya afya hutolewa kwa watu;
- Mazingira ya huduma ya afya kwa mifugo;
- Mashirika ya udhibiti wa wanyama;
- Mashirika ya kibinadamu yasiyo ya faida; na
- Sehemu za mauzo ya rejareja ya bangi, zikiwa pamoja na mahali ambapo watoa ushauri wa matibabu ya bangi hutoa huduma zao.

Iwapo kituo cha afya kinahitaji barakoa nje ya nyumba, ni lazima ufuata kanuni zao za biashara. Tazama taarifa ya "[kanuni za chumba](#)" iliyo hapo juu ili kupata taarifa zaidi. Tafadhali tembelea ukurasa wa [Uzuiaji wa Maambukizo ya COVID-19 katika Mazingira ya Huduma ya Afya](#) (Kiingereza pekee) ili kupata mwongozo wa kina ukiwemo [mwongozo wa udhibiti wa chanzo](#) (Kiingereza pekee) na mwongozo wa kutembelea vituo fulani vya utunzaji wa afya.

### **Kanuni za Chumba**

Biashara, mashirika, vituo, na sehemu zina haki ya kuweka kanuni zao za kuvala barakoa katika sehemu au kituo chao. Biashara zinahitajika kufuata mahitaji yote katika [mahitaji ya L&I](#) (Kiingereza pekee) na wanaweza kuchagua kuhitaji barakoa katika mazingira (mfano nje ya nyumba) ili kuwa ya kinga zaidi ya [Amri ya Barakoa ya Katibu wa Afya](#) (Kiingereza pekee).

Maafisa wa afya ya umma ya ndani pia huenda wakawenza amri za kinga za barakoa ili kubana msambao katika jamii. Kanuni hizi zinaweza kuleta kinga zaidi ya [Amri ya Barakoa ya Katibu wa Afya](#) (Kiingereza pekee), lakini haziwezi kuwa na utunzaji kiasi.

Isitoshe, baadhi ya watu huenda wakahitaji, au kuchagua, kuendelea kuvala barakoa. Wana haki ya kuchagua kuvala barakoa wakiwa kwa umma hata kama sheria za jimbo au za ndani za kuvala barakoa hazifanyi kazi. Tafadhali heshimu chaguo lao la kuvala barakoa ili kujilinda, kulinda familia na jamii zao. Kumbuka kuwa ukichagua kuvala barakoa unaweza kuomba kuitoa kwa muda mfupi katika hali kama vile hali za malengo ya utambulisho.